
Muhtasari

# Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu **2013**

## Kuinuka kwa Nchi za Kusini:

Maendeleo ya Binadamu katika Ulimwengu Anuwai



Hati ya kunakili © 2013
na Mradi wa Maendeleo ya Umoja wa Mataifa
1 UN Plaza, New York, NY 10017, USA

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutoa tena sehemu yoyote ya chapisho hili, kuhifadhi au kuwasilisha, katika umbo lolote au kwa namna yoyote ile, kielektroniki, kwa kutumia mitambo, kwa kunakili, kurekodi au vinginevyo, bila idhini ya awali.

Kimehaririwa na kutolewa na: Communications Development Incorporated, Washington DC
Kimesanifiwa na: Melanie Doherty Design

For a list of any errors or omissions found subsequent to printing, please visit our website at http://hdr.undp.org

# Timu ya Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu 2013

### Mkurugenzi na mwandishi mkuu

Khalid Malik

### Utafiti na takwimu

Maurice Kugler (Mkuu wa Utafiti), Milorad Kovacevic (Mtakwimu Mkuu), Subhra Bhattacharjee, Astra Bonini, Cecilia Calderón, Alan Fuchs, Amie Gaye, Iana Konova, Arthur Minsat, Shivani Nayyar, José Pineda and Swarnim Waglé

### Mawasiliano na uchapishaji

William Orme (Mkuu wa Mawasiliano), Botagoz Abdreyeva, Carlotta Aiello, Eleonore Fournier-Tombs, Jean-Yves Hamel, Scott Lewis and Samantha Wauchope

### Utendaji na utawala

Eva Jespersen (Meneja Mtendaji), Christina Hackmann, Jonathan Hall, Mary Ann Mwangi and Paola Pagliani

### Ofisi ya Ripoti za Maendeleo ya Binadamu

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ni zao la juhudi za pamoja chini ya uongozi wa Mkurugenzi, pamoja na wafanyakazi wa utafiti na takwimu; mawasiliano na uchapishaji; na timu inayosaidia Ripoti za Maendeleo ya Binadamu. Wenzetu wa utendaji na utawala husaidia katika kazi za ofisini.

## Muhtasari

# Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu 2013

## Kuinuka kwa Nchi za Kusini:

## Maendeleo ya Binadamu katika Ulimwengu Anuwai

Published for the
United Nations
Development
Programme
(UNDP)

*Empowered lives.*
*Resilient nations.*

# Dibaji

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu 2013, *Kuinuka kwa Nchi za Kusini: Maendeleo ya Binadamu katika Ulimwengu Anuwai,* huangazia mabadiliko ya siasa ya nchi kama inavyoathiriwa na jiografia wakati huu, ikichunguza maswala ibuka na mitindo na pia wahusika wapya wanaobadilisha uwanja wa maendeleo.

Ripoti hii inatoa hoja kwamba mabadiliko yanayofanana yanayotokea katika idadi kubwa ya nchi zinazoendelea na kuzifanya kuwa nchi zenye uchumi mkubwa wenye ushawishi wa kisiasa unaokua imekuwa na athari kubwa kwenye ukuzaji wa maendeleo ya binadamu.

Ripoti hii inaeleza kuwa katika mwongo uliopita nchi zote zilichapuza mafanikio yake katika elimu, afya, na kiwango cha mapato kama ilivyokadiriwa katika Kielezo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) – hivi kwamba hakuna nchi ambayo data yake ilikuwepo ilikuwa na thamani ya chini ya HDI katika mwaka 2012 kuliko ilivyokuwa mwaka 2000. Jinsi maendeleo ya kasi yalivyoafikiwa katika nchi za HDI ya chini katika kipindi hiki, ndivyo kulikuwa na kukaribiana kunakotambulika kwa thamani za HDI ulimwenguni, ingawa maendeleo yalitofautiana kwenye na kati ya maeneo.

Kwa kuangazia nchi ambazo ziliinua thamani yake ya HDI kwa kiasi kikubwa kati ya 1990 na 2012 katika vipengele vya maendeleo ya binadamu vya mapato na visivyo vya mapato, Ripoti hii inachunguza mbinu zilizowezesha nchi hizo kufanya vyema. Kwa namna hiyo, Ripoti hii ya 2013 inatoa mchango mkubwa kwa fikra za kimaendeleo kwa kueleza vipengele mahususi vya kubadilisha maendeleo na kupendekeza sera za baadaye zinazopasa kupewa kipaumbele na ambazo zinaweza kusaidia kuendeleza msukumo huo.

Kufikia 2020, kwa mujibu wa makadirio yaliyokuziwa Ripoti hii, matokeo ya kiuchumi yaliyounganishwa ya nchi tatu pekee zinazoendelea – Brazili, Uchina na India – yatazidi jumla ya uzalishaji wa Kanada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Uingereza na Marekani. Upanuzi huu, kwingi unaendeshwa na ubia wa biashara na teknolojia mpya katika nchi za Kusini. Hivyo ndivyo Ripoti hii inavyoonyesha pia.

Hata hivyo, ujumbe muhimu ulio katika hii Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu na zile za awali ni kwamba ukuaji wa kiuchumi pekee hauchangii kiotomatiki ukuaji wa maendeleo ya binadamu. Sera zinazotetea maskini na uwekezaji wenye maana katika uwezo wa watu – kupitia kwa kusisitiza elimu, lishe na afya, na ujuzi wa ajira – zaweza kupanua upatikanaji wa kazi nzuri na ziwezeshe kuwepo kwa maendeleo endelevu.

Ripoti ya 2013 inatambua maeneo manne mahususi ya kuzingatiwa ili kuendeleza msukumo wa maendeleo: kuzidisha usawa, ikiwa ni pamoja na kipengele cha jinsia; kuwezesha kusikika zaidi na kushiriki kwa wananchi, kujumuisha vijana, kukabiliana na shinikizo za kimazingira; na kusimamia mabadiliko ya kidemografia.

Ripoti hii pia inapendekeza kwamba jinsi changamoto za maendeleo ulimwenguni zinavyokuwa changamani zaidi na zinazovuka mipaka, vitendo vilivyoratibiwa juu ya changamoto za enzi yetu zinazohitaji suluhu ya haraka, hata kama ni umalizaji wa umaskini, mabadiliko ya tabianchi, au amani na usalama, ni muhimu. Jinsi nchi zinavyoingiliana kupitia kwa biashara, uhamiaji, teknolojia za habari na mawasiliano, si jambo la kustaajabisha kwamba maamuzi ya sera yanayotolewa mahali pamoja huwa na athari kubwa kwingineko. Matatizo makuu ya miaka ya hivi karibuni – chakula, uchumi, tabianchi – ambayo yameangamiza maisha ya wengi huelekeza kwa hilo, na pia kwa umuhimu wa kujitahidi kupunguza urahisi wa watu kukumbwa na mashambulizi makali na majanga.

Ili kutumia vyema ufahamu, ujuzi, na fikra za kimaendeleo zilizo Kusini, Ripoti hii inasema kuwa kuanzishwa taasisi mpya ambazo zitawezesha muungano wa kimaeneo na ushirikiano wa Kusini-Kusini. Tayari mataifa yenye uwezo yanayoibuka katika ulimwengu unaokua ni vyanzo vya uvumbuzi wa sera za kijamii na kiuchumi na pia ni wafanyabiashara wakuu, wawekezaji, na washirika wa

uhusiano wa kimaendeleo wa nchi nyingine zinazoendelea.

Nchi nyingi nyingine zilizo Kusini zimestawi kwa haraka, na hivyo tajriba zao na ushirikiano wa Kusini-Kusini pia ni msukumo wa kutosha kuwa na sera ya maendeleo. UNDP imeweza kutekeleza wajibu muhimu kama wakala wa habari na ufahamu, na kama mwalikaji wa wabia – serikali, makundi ya kijamii na makampuni ya kimataifa – ili wabadilishane tajriba zao. Pia tuna wajibu muhimu w kuwezesha ujifunzaji na ujenzi wa watu wenye ujuzi. Ripoti hii inatoa umaizi muhimu wa namna ya kujihusisha katika ushirikiano wa Kusini-Kusini siku za usoni.

Hatimaye, Ripoti hii pia inatualika kuangazia kwa makini taasisi za kiutawala ulimwenguni ili kukuza dunia ya haki na usawa. Inabainisha miundo ambayo imepitwa na wakati na ambayo haiakisi uhalisia mpya wa kiuchumi na kijiografia ulioelezwa, na inazingatia mambo ya kuchaguliwa wakati wa kipindi cha ubia mpya. Pia inaomba kuwepo na uwazi na uwajibikaji mkubwa, na inasisitiza jukumu la makundi ya kijamii ulimwenguni katika kutetea hili na uwezo mkubwa wa kufanya maamuzi wa wale walioathiriwa moja kwa moja na changamoto za kilimwengu. Hawa mara nyingi huwa ni wale watu fukara kabisa na wanaoweza kudhuriwa kwa urahisi katika ulimwengu wetu.

Huku mazungumzo kuhusu ajenda ya maendeleo ya ulimwengu baada ya 2015 yakiendelea, ninatumai kwamba watu wengi watapata muda wa kuisoma Ripoti hii na kutafakari juu ya mafunzo yake kwa ulimwengu wetu unaobadilika kwa haraka. Ripoti hii inaleta nguvu mpya katika uelewa wetu wa hali ya sasa ya maendeleo ya ulimwengu. Pia inadhihirisha kiasi ambacho watu wanaweza kujifunza kutokana na tajriba ya ukuaji wa haraka unaoonekana katika nchi nyingi za Kusini.



Helen Clark
*Administrator*
United Nations Development Programme

# Muhtasari wa HDR 2013

Wakati nchi zilizoendelea zilikoma kukua katika kipindi cha matatizo makuu ya kiuchumi yaliyotokea 2008 – 2009 lakini nchi zinazoendelea zikazidi kukua, ulimwengu wote uliamka. Kuinukia kwa Kusini, kulikochukuliwa na ulimwengu unaoendelea kama kama namna ya usawazishaji wa dunia, umezungumziwa sana tangu wakati huo. Mazungumzo haya yamejikita kwa namna finyu kwenye GDP na ukuaji wa biashara katika nchi chache kubwa; ingawa kuna mambo mengi yanayohusika, yanayahusu nchi nyingi zaidi na mielekeo ya kina yenye athari kubwa kwa maisha ya watu, kwa usawa wa kijamii na kwa utawala wa kidemokrasia katika viwango vya mahali maalumu na ulimwengu mzima. Kama Ripoti hii inavyoonyesha, kuinukia kwa Kusini ni swala la uwekezaji mfululizo katika maendeleo na mafanikio ya binadamu na pia ni nafasi ya ukuaji zaidi wa binadamu katika ulimwengu kwa jumla. Kuufanya ukuaji huo kuwa wa hakika kutahitaji utungaji sera uliokita kwenye ufahamu na elimu ulimwenguni na kitaifa, ukifaidi kutoka kwa mafunzo ya sera yaliyochanganuliwa katika ripoti hii.


## Kuinuka kwa Kusini

Kuinuka kwa Kusini hakuna mfano katika ile kasi na ukubwa wake. Inabidi ieleweke katika muktadha mpana wa maendeleo ya binadamu kama kisa cha upanuzi wa kuvutia wa uwezo wa watu binafsi na ukuaji mfululizo wa maendeleo ya binadamu katika nchi ambazo kunaishi idadi kubwa ya watu wa dunia hii. Wakati nchi nyingi na mabilioni ya watu wanapokwea ngazi ya maendeleo, kama wanavyofanya sasa, hili huwa na athari ya moja kwa moja kwenye uzalishaji mali na ukuaji mpana wa binadamu katika nchi na maeneo yote ulimwenguni. Kuna nafasi mpya kwa nchi ambazo hazijaendelea sana kuzifikia zile zilizoendelea, na pia ya kuanzisha sera bunifu ambazo zingefaidi hata nchi zenye uchumi ulioendelea pia.

Ingawa karibu nchi zote zinazoendelea zimefanikiwa, kuna idadi kubwa ya nchi zilizofanikiwa sana – na hii ndiyo inayoweza kuitwa "kuinuka kwa Kusini". Baadhi ya nchi kubwa zimepata mafanikio ya haraka, na zinazotambulika sana ni Brazili, Uchina, Indonesia, Meksiko, Afrika Kusini na Uturuki. Lakini kumekuwepo pia maendeleo ya haja katika nchi zenye uchumi mdogo kama Bangiladeshi, Chile, Ghana, Morisi, Rwanda, Tailandi na Tunisia (kielelezo 1).

KIELELEZO 1

**Zaidi ya nchi 40 za Kusini zilipata ongezeko kubwa kabisa la thamani ya HDI kati ya mwaka 1990 na mwaka 2012 kuliko ilivyobashiriwa ukizingatia thamani yao ya HDI ya mwaka 1990**





**Kumbuka:** Nchi zilizo juu ya laini ya digrii 45 zilikuwa na thamani ya juu ya HDI mwaka 2012 kuliko mwaka 1990. Alama za rangi ya kijivu na nyeusi zinaashiria nchi zenye ongezeko kubwa kabisa la thamani ya HDI kati ya mwaka 1990 na mwaka 2012 kuliko ulivyobashiriwa ukizingatia thamani yao ya HDI ya mwaka 1990. Nchi hizi zilitambulishwa kwa misingi ya mabaki yaliyopatikana kutoka kupungua kwa mabadiliko katika logi ya HDI kati ya mwaka 2012 na mwaka 1990 kwenye logi ya 1990. Nchi zilizotajwa ni kundi lililochaguliwa la viboresha HDI kwa haraka ambazo zimezungumziwa kwa kina katika sura 3.
**Chanzo:** kokotoo ya HDRO.

Huku ikiwa inasisitiza kuinuka kwa Kusini na athari yake kwa maendeleo ya binadamu, *Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu* 2013 pia inahusu ulimwengu huu unaobadilika, ikiendeshwa kwa kiwango kikubwa na kuinuka kwa Kusini. Inachunguza hatua za maendeleo zilizopigwa, changamoto zinazojitokeza (baadhi zikiwa ni matokeo ya ufanisi huo) na nafasi zinazoibuka za utawala wakilishi wa ulimwengu mzima na wa kimaeneo.

Kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 150, mazao jumla ya nchi tatu zenye uchumi unaoongoza katika ulimwengu unaoendelea – Brazili, Uchina na India – ni karibu sawa na GDP jumla ya mataifa ya Kaskazini yenye uwezo wa kiviwanda kwa muda mrefu – Kanada, Ufaransa, Ujerumani, Italia, Uingereza na Marekani. Hali hii inawakilisha usawazishaji mkubwa wa nguvu za kiuchumi ulimwenguni. Mnamo mwaka 1950 Brazili, Uchina na India, kwa pamoja, ziliwakilisha 10% ya uchumi wa ulimwengu, huku nchi sita za Kaskazini ambazo kwa desturi zilikuwa viongozi wa uchumi ziliwakilisha zaidi ya nusu. Kwa mujibu wa ubashiri ulio katika Ripoti hii, kufikia 2050 Brazili, Uchina na India kwa pamoja zitawakilisha 40% ya mazao ya dunia (kielelzo 2), zikipiku mazao ya jumla yaliyobashiriwa ya jumuiya ya Kundi la Saba la sasa.

KIELELZO 2

**Imebashiriwa kwamba Brazili, Uchina na India kwa pamoja zitawakilisha 40% ya mazao ulimwenguni kufikia 2050, ikiwa ni ongezeko kutoka 10% mnamo mwaka 1950**





Kumbuka: Mazao yamepimwa kwa uwezo uliosawazishwa wa kununua dola kama ilivyokuwa mwaka 1990.

Chanzo: Data ya kihistoria kutoka Maddison (2010) iliyoongezewa na HDRO na ubashiri ulioegemezwa kwenye Pardee Center for International Futures (2013).

Huko Kusini, tabaka la kati huko linakuwa haraka sana katika ukubwa, mapato na matarajio (kielelezo 3). Idadi ya watu pekee walio Kusini – mabilioni ya wanunuzi na wananchi – huzidisha athari ya vitendo vya maendeleo ya binadamu ulimwenguni na serikali, kampuni na taasisi za kimataifa huko Kusini. Hivi sasa Kusini inajitokeza sambamba na Kaskazini kama mahali pa kuelimisha watu kuhusu uvumbuzi wa kiteknolojia na ubunifu wa ujasiriamali. Katika biashara ya Kaskazini-Kusini, nchi mpya zinazopitia uchumi wa kiviwanda zimejenga uwezo wa kutengeneza bidhaa changamano kwa ajili ya masoko ya nchi zilizoendelea. Lakini kuingiliana kwa Kusini-Kusini kumewezesha kampuni za Kusini kuchukua na kutumia upya bidhaa na michakato ambayo inafaa mahitaji ya mahali hapo.

KIELELEZO 3

**Tabaka la kati lililo Kusini limepigiwa upatu kuzidi kukua**




**Kumbuka:** Tabaka la kati linajumuisha watu wanaopata au kutumia $10-$100 kwa siku (kulingana na uwezo uliosawazishwa wa kununua katika mwaka 2005)
**Chanzo:** Brookings Institution 2012.

## Hali ya maendeleo ya binadamu

Katika mwaka 2012, Kielezo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI) kinafichua kuwa hatua kubwa imepigwa. Katika miongo iliyopita nchi kote ulimwenguni zimekuwa zikikaribiana katika kufikia viwango vya juu vya maendeleo ya binadamu. Mwendo wa maendeleo ya HDI umekuwa wa kasi sana katika nchi zilizo kwenye kategoria za chini na wastani za maendeleo ya binadamu. Hizi ni habari njema. Hata hivyo ukuaji huhitaji zaidi ya mafanikio ya wastani katika HDI. Halitakuwa jambo la kufurahia wala linaloweza kuendelezwa ikiwa ongezeko la HDI linaambatana na ongezeko la kutokuwa na usawa katika mapato,ruwaza za utumiaji zisizoweza kuendelezwa, matumizi ya juu ya jeshi na uwiano wa kijamii (angalia kisanduku 1)

Sehemu muhimu ya maendeleo ya binadamu ni usawa. Kila mwanadamu ana haki ya kuishi maisha makamilifu kulingana na na maadili na matamanio yake. Hakuna mtu atakayehukumiwa maisha mafupi au yenye taabu kwa kuwa anatoka tabaka au nchi "isiyo sahihi", kabila au jamii "isiyo sahihi" au jinsia "isiyo sahihi". Kutokuwa sawa hupunguza kasi ya maendeleo ya binadamu na wakati mwingine kunaweza kuyazuia kabisa. Kwa jumla, kutokuwa sawa kumepungua kwa kiasi kikubwa katika afya na elimu katika miongo miwili iliyopita kuliko katika mapato (kielelezi 4). Karibu tafiti zote zinaafikiana kwamba hali ya kutokuwa sawa kimapato iko juu kote ulimwenguni, ingawa hakuna makubaliano kuhusu mielekeo ya hivi karibuni.

## Kusini ya kiulimwengu zaidi

Uzalishaji ulimwenguni unajisawazisha tena kwa namna ambazo hazijaonekana katika miaka 150. Ongezeko la uvushaji wa bidhaa kwenye mipaka, huduma, watu na mawazo halina kifani.Kufikia mwaka 2011, biashara iliwakilisha karibu 60% ya mazao yote duniani. Nchi zinazoendelea zilitoa mchango mkubwa katika hili (kisanduku 2): kati ya 1980 na 2010 ziliongeza mgao wake wa bidhaa za kibiahsara ulimwenguni kutoka 25% hadi 47% na

*Amartya Sen, Mshindi wa Tuzo ya Nobel ya Uchumi*

**Inahisije kuwa binadamu?**

Karibu nusu karne iliyopita hiiv, mwanafalsafa Thomas Nagel alichapisha makala maarufu iliyoitwa "What Is It Like to Be a Bat?" ("Inahisije kuwa popo?") Swali ninalotaka kuuliza ni hili: inahisije kuwa mwanadamu? Kama inavyotokea, makala maizi ya Tom Nigel iliyochapishwa katika The Philosophical Review yalikuwa pia yanahusu binadamu, na kwa kiasi kidogo tu popo. Pamoja na hoja zingine, Nagel alieleza shaka za kina kuhusu jaribio la wanasayansi wa kiuchunguzi kubainisha tajriba ya kuwa popo – au vivyo hivyo, mwanadamu – pamoja na tukio la kimaumbile linalohusishwa katika ubongo na kwingineko mwilini, ambayo yanaweza yakafikiwa kwa urahisi na ukaguzi wa nje.Dhana ya kuwa popo au binadamu haiwezi kuonekana kama kuwa na mtetemo fulani katika ubongo na mwilini. Uchangamano wa hali hiyo ya kwanza hauwezi kutatuliwa na usikivu unaokuja kwa wepesi wa hiyo ya pili (hata kama inashawishi sana kufanya hivyo).

Mtazamo wa hivi punde wa maendeleo ya binadamu umejengwa kwenye utofautishaji – lakini wa aina tofauti na ukinzano wa epistomolojia ya kimsingi wa Nagel. Mtazamo ambao Mahbub-ul-Haq aliasisi katika mfululizo wa Human Development Reports (Ripoti za Maendeleo ya Binadamu) ulioanza 1990 ni ule ulio kati ya, kwa upande mmoja, tatizo gumu la kukadiria ukwasi wa maisha ya binadamu, ikiwa ni pamoja na uhuru ambao binadamu wana sababu za kuthamini, na kwa upande mwingine, zoezi rahisi zaidi la kufuatilia mapato na rasilmali za nje ambazo watu – au mataifa – huwa nazo. Ni rahisi zaidi kupima GDP kuliko kupima ubora wa maisha ambao watu wanao. Lakini hali njema na uhuru wa binadamu, na kufungamana kwao na haki humu ulimwenguni hakuwezi kupunguzwa na kulinganishwa na upimaji wa GDP na kiwango chake cha ukuaji, kama watu wengi wanavyoshawishika kufanya.

Uchangamano halisi wa maendeleo ya binadamu ni muhimu katika kukubali, kwa kiasi fulani kwa sababu hatustahili kupotoshwa kulibadilisha swali: hii ndiyo ilikuwa hoja kuu iliyoongoza harakati shupavu za Mahbub-ul-Haq kujaliza – na kwa kiasi fulani kutwaa mahali pa – GDP. Lakini pamoja na hayo kulitokea hoja ngumu zaidi ambayo pia ni sehemu isiyoweza kuepukwa ya kile ambacho kimekuja kujulikana kama "mtazamo wa maendeleo ya binadamu". Tunaweza, kwa ajili ya kurahisisha mambo, kutumia ishara nyingi rahisi za maendeleo ya binadamu kamaHDI, kutegemea vigezogeu vitatu tu pamoja na sheria rahisi ya kuvikadiria – lakini uchunguzi hauwezi kuishia hapo. Tusipuuze njia za mkato zinazofanya kazi na zinazofaa – HDI yaweza kutueleza mengi kuhusu ubora wa maisha ya binadamu kuliko inavyofanya GDP – lakini tusiridhike kabisa na manufaa ya haraka yanayopatikana kupitia njia hizi za mkato katika ulimwengu wa mazoezi mfululizo. Kukadiria ubora wa maisha ni zoezi changamano zaidi kuliko kinachoweza kunaswa na nambari moja pekee, hata kama uchaguzi wa vigezogeu vitakavyohusishwa umefanywa kwa busara na uchaguzi wa utaratibu wa kukadiria vivyo hivyo.

Utambuzi wa uchangamano una athari nyingine muhimu pia. Dhima muhimu ya urazini wa umma, ambao Ripoti ya Mwaendeleo ya Binadamu ya sasa inasisitiza, unatokea kwa kiasi kutokana na utambuzi wa uchangamano huu. Siri ya mtungi aijuaye kata, lakini mipango ya kuepuka siri hiyo haiwezi kushughulikiwa vyema bila kuwapa wananchi uwezo wa kuamua na pia kuwapa nafasi za kutosha za kuwa na mjadala wa umma. Umuhimu wa vipengele tofauti katika kutathmini hali njema na uhuru wa watu unaweza kutambuliwa vyema na kukadiriwa kupitia tu kwa mijadala baina ya watu, ukiwa na athari ya utengenezaji wa sera ya umma. Umuhimu wa kisiasa wa ari ya kuanzisha mambo kama Arab Spring, na ushirikiano wa watu wengi kwingineko humu ulimwenguni, unalingana na ufahamu wa umuhimu wa watu kujieleza kwa kujadili na wengine kuhusu matatizo yaliyopo katika maisha yao na udhalimu wanaotaka kuondoa. Kuna mengi ya kujadili - baina ya wahusika wote na pamoja na watumishi wa umma wanaounda sera.

Jukumu hili la kubadilishana mawazo, linapotambuliwa vyema na wahusika wote wa utawala, lazima pia lijumuishe uwakilishaji wa maslahi ya watu wasiokuwepo hapa ili kueleza masikitiko yao kwa sauti zao wenyewe. Haiwezekani maendeleo ya binadamu kutojali vizazi vijavyo kwa kuwa tu bado havipo hapa. Lakini binadamu wana uwezo wa kufikiri kuhusu wengine, na maisha yao, na sanaa ya siasa ya uaminifu na uwajibikaji ni kupanua mijadala kutoka ufinyu wa kufikiria juu ya maslahi yao wenyewe tu hadi uelewa mpana wa kijamii unaohusu mahitaji na uhuru wa watu wakati ujao pamoja na leo. Hili si swala la kujumuisha tu maslahi hayo katika kiashirio kimoja – kwa mfano, kwa kusonga HDI ambayo tayari ina mzigo mzito (ambayo inasimamia, kwa namna yoyote ile, hali njema na uhuru wa sasa tu) – lakini bila shaka hili ni swala la kuhakikisha kuwa mjadala kuhusu maendeleo ya binadamu yanajumuisha maslahi hayo mengine. Ripoti za Maendeleo ya Binadamu zinaweza kuendelea kuchangia upanuaji huu kupitia maelezo pamoja na uwasilishaji wa majedwali yenye habari husika.

Mtazamo wa maendeleo ya binadamu ni hatua kubwa mbele katika zoezi gumu la kuelewa ufanisi na mapungufu ya maisha ya binadamu, na pia katika kutambua umuhimu wa tafakuri na mijadala, na kupitia kwa hayo kuendeleza haki ulimwenguni. Tunaweza kuwa tunafanana na popo sana katika kutofikika kwa urahisi na kipimo cha mwanasayansi wa kiuchunguzi asiye subira, lakini tuna uwezo wa kufikiri na kuzungumza kuhusu desturi ya maisha yetu kuwa na sura nyingi na ile ya wengine – leo na kesho – kwa njia ambazo haziwezi kupatikana moja kwa moja kwa popo. Kuwa mwanadamu ni sawa na kuwa kama popo na pia kutokuwa kama popo.


ways that may not be readily available to bats. Being a human being is both like being a bat and very unlike it.

mgao wake wa ulimwenguni kutoka 33% hadi 45%. Pia nchi zinazoendelea zimekuwa zikiimarisha uhusiano wao wenyewe kwa wenyewe. Kati ya 1980 na 2011, biashara ya Kusini-Kusini, kama mgao wa bidhaa za kibiashara ulimwenguni, ilipanda kutoka 8.1% hadi 26.7% (kielelezo 5).

Kuinuka kwa Kusini hakujalingana katika nchi zote zinazoendelea. Kwa mfano, mwendo wa mabadiliko ni wa polepole katika nyingi ya nchi 48 zenye maendeleo ya chini kabisa, hususan zile ambazo hazina bandari au zilizo mbali na masoko ya dunia. Hata nivyo, nyingi ya nchi hizi zimeanza kunufaika na biashara ya Kusini-Kusini,

KIELELEZO 4

**Maeneo mengi yanaonyesha ongezeko la kutokuwa sawa katika mapato na kupungua kwa kutokuwa sawa katika afya na elimu**




**Kumbuka:** Based on a population-weighted balanced panel of 182 countries for loss due to health inequality, 144 countries for loss due to education inequality and 66 countries for loss due to income inequality. Data kuhusu kutokuwa sawa kwa mapato kutoka Milanovic(2010) inapatikana hadi mwaka 2005.
**Chanzo:** Kokotoo za HDRO zinazotumia data ya afya kutoka majedwali ya maisha ya Idara ya Umoja wa Mataifa ya Uchumi na Maswala ya Kijamii, data ya elimu kutoka Barro na Lee (2010) na data ya kutokuwa na mapato sawa kutoka Milanovic(2010).

uwekezaji, usimamizi wa fedha na uhamisho wa teknolojia.Kwa mfano, kumekuwepo na ongezeko la ziada kutoka Uchina hadi nchi zinazoendelea, hususan wabia wa karibu wa kibiashara. Kwa kiasi fulani manufaa haya yamefidia upungufu wa mahitaji kutoka kwa nchi zilizoendelea. Ukuaji katika nchi za mapato ya chini ungekadiriwa kuwa pointi 0.3-1.1% chini mwaka 2007-2012 kama ukuaji ungepungua katika kiwango sawa nchini Uchina na India kama ilivyo katika nchi zenye uchumi ulioendelea.

Nchi nyingi pia zimeidi kutokana na ziada inayoingia katika sekta ambazo zinachangia maendeleo ya binadamu, hasa afya. Kwa mfano, kampuni za India zinatoa madawa ya bei nafuu, vifaa vya kitabibu, bidhaa na huduma za mawasiliano na teknolojia kwa nchi za Afrika. Kampuni za Brazili na Afrika Kusini zinafanya vivyo hivyo katika masoko ya maeneo yao.

Hata hivyo, bidhaanje kutoka kwa nchi kubwa zaweza kuwa na upungufu wake. Nchi kubwa huzua shinikizo za ushindani katika nchi ndogo ambazo zinaweza kuzuia uanuai wa kiuchumi na kiviwanda. Hata hivyo, pia kuna hali ambapo mishtuko ya ushindani imefuatwa na ufufuaji wa kiviwanda. Dhima ya ushindani leo inaweza kubadilika kwa urahisi sana na kuwa dhima ya kukamilishana kesho. Inaonekana kwamba kutoka kwa ushindani na kwenda kwa kushirikiana hutegemea sera zinazoshughulikia changamoto mpya.

KISANDUKU 2

**Utangamano wa Kusini na uchumi wa ulimwengu na maendeleo ya binadamu**


Mnamo 1990 – 2010, katika sampuli ya nchi 107 zinazoendelea, inaweza kuchukuliwa kwamba takriban 87% ya nchi hizo zina utangamano wa kiulimwengu; ziliongezaziliongeza kiwango cha mazao yao ya biashara, zina washirika wengi wakubwa wa kibiashara1 na wanahifadhi kiwango kikubwa cha mazao ya kibiashara ikilinganishwa na nchi zenye mapato sawa.2 Nchi hizi zote zinazoendelea pia zimeunganishwa kwa kiasi kikubwa na ulimwengu na kila moja na nyingine. Matumizi ya mtandao yamepanuka sana, huku kiwango cha kati cha ukuaji wa watumiaji kila mwaka kikizidi 30% kati ya mwaka 2000 na 2010.

Ingawa si nchi zote zinazoendela zenye utangamano wa kiulimwengu zilizopigz hatua kwenye Kielezo cha Maendeleo ya Binadamu (HDI), kinyume chake ni kweli. Karibu nchi zote zinazoendelea ambazo zilifanya vizuri zaidi katika HDI zikilinganishwa na nyingine zinazofanana nazo kati ya 1990 na 2012 (angalau 45 katika sampuli iliyo hapa) zimetangamana zaidi na uchumi wa dunia katika miongo miwili iliyopita. Ongezeko lao la wastani katika uwiano wa biashara na mazao ni kama pointi 13% zaidi ya kundi la nchi zinazoendelea zenye mafanikio kiasi upande wa HDI. Hii inalingana na matokeo ya awali kwamba nchi huelekea uwazi zaidi jinsi zinavyokua.3

Nchi nyingi zenye utangamano zilizofanya vyema sana katika HDI hujumuisha sit u zile kubwa ambazo hutawala vichwa vya habari, lakini pia idadi kubwa ya nchi ndogo na ambazo zina maendeleo madogo sana. Kwa hiyo zinaunda kundi kubwa anuwai kuliko zenye uchumi wa kibiashara zinazoinukia ambazo hujulikana kwa akronimu kama BRICS (Brazili, Shirikisho la Urusi, India, Uchina na Afrika Kusini), IBSA (India, Brazili na Afrika Kusini), CIVETS (Kolombia, Indonesia, Vietnamu, Misri, Uturuki na Afrika Kusini) na MIST (Meksiko, Indonesia, Korea Kusini [Jamhuri ya Korea] na Uturuki).

Kielelezo kilicho hapa chini kinachora uboreshaji katika HDI4 dhidi ya mabadiliko katika wiano wa biashara na mazao, kiashirio cha kina cha ushiriki katika masoko ya dunia. Zaidi ya humusi nne ya nchi hizi zinazoendelea iliongeza uwiano kati ya biashara na mazao kati ya 1990 na 2012. Kati ya vighairi katika kikundi kidogo ambazo pia zilipztz uboreshaji mkubwa wa HDI ni Indonesia, Pakistani na Venezuela. Hizi ni nchi tatu kubwa ambazo zinachukuliwa kuwa zinatamba katika ulimwengu wa masoko, zikifanya biasharanje au kuingiza bidhaa kutoka nchi zisizopungua 80. Nchi mbili ndogo ambazo uwiano kati ya biashara na mazao ulipungua (Morisi na Panama) zaendelea kufanya biashara katika viwango vya juu zaidi kuliko ilivyotarajiwa kwa nchi zenye viwango hivyo vya mapato. Nchi zote ambazo ziliboresha HDI kwa kiasi kikubwa na zikaongeza uwiano kati ya biashara na mazao kati ya 1990 na 2012 zimeonyeshwa kwa wino tofauti katika roboduara iliyo juu kulia mwa kielelezo. Nchi zilizo katika roboduara ya chini kulia (pamoja na Kenya, Ufilipino na Afrika Kusini) ziliongeza wiano kati ya biashara na mazao lakini zikaboresha HDI kwa kiasi cha haja tu.

Maendeleo ya binadamu na upanuzi  wa biashara Kusini




1. Biashara ya pande mbili inayozidi $2 million katika 2010–2011.
2. Imetegemea matokeo kutoka wiano wa kupungua kwa biashara katika nchi nyingi na GDP kuhusu mapato ya mtu mmoja ambayo yanadhibiti idadi ya watu na kutokuwa na bandari.
3. Tazama Rodrik (2001).
4. Uboreshaji wa HDI unapimwa na mabaki kutoka kwa kupungua kwa mabadiliko katika logi ya HDI kati ya 1990 na 2012 kwenye logi ya HDI ya mwanzo ya mwaka 1990. Nchi tano zilizoonyeshwa kwa wino wa rangi ya kijivu upande wa juu kushoto wa roboduara ziliboresha HDI sana lakini zikapunguza wiano wa biashara na mazao kati ya 1990 na 2010, ingawa zilihifadhi idadi kubwa ya ushirikiano mkubwa wa kibiashara ulimwenguni au zilifanya biashara zaidi kuliko ilivyobashiriwa kwa nchi zenye kiwango sawa cha mapato ya kila mtu. Nchi ambazo zilionyeshwa kwa wino wa rangi ya kijivu upande wa juu kulia na upande wa chini kulia wa roboduara ziliboresha HDI kwa kiwango cha wastani kati ya 1990 na 2012 lakini ziliongeza wiano wao wa biashara na mazao au walikuwa na idadi kubwa ya uhusiano wa kibiashara.
**Chanzo:** kokotoo za HDRO; wiano wa biashara na mazao kutoka Benki ya Dunia (2012a).

## Viendesha mageuzo ya maendeleo

Katika miongo miwiwli iliyopita, nchi nyingi zimepiga hatua kubwa: kuinuka kwa Kusini kumejumuisha mambo mengi. Hata hivyo,watu kadhaa wakuu hawajaongezea tu mapato ya kitaifa, lakini wao pia walikuwa na utendaji mzuri kwenye viashirio kama afya na elimu (kielelezo 6).


Nchi nyingi za Kusini zimewezaje zimebadilisha vipi matamanio yao ya maendeleo ya binadamu? Katika nyingi ya nchi hizi, kumekuwepo na viendesha maendeleo vinavyotambulika: hali changamfu ya kimaendeleo, kutumia masoko ya kiulimwengu na kupambanua sera ya kijamii na uvumbuzi. Viendesha hivi havijatolewa kutoka mambo ya kidhahania ya jinsi maendeleo yanatakiwa kufanya kazi; ila, vinadhihirishwa na tajriba za maendeleo ya kiugeuzi ya nchi nyingi Kusini. Kwa kweli, wanatoa changamoto kuhusu mitazamo iliyowazwa kabla na ile inayoelekeza. Kwa upande mmoja wanatenga idadi fulani ya kiujima, maadili yanayoshughulikiwa kutoka mahali pamoja; na kwa upande mwingine, wanaacha fikra huru zilizoungwa mkono na Washington Consensus.

### Kiendesha 1: mataifa yaliyokubali wajibu

Taifa lenye nguvu, tendaji na linalowajibika hukuza sera kwa ajili ya sekta za umma na za kibinafsi – kutegemea maono na uongozi wa muda mrefu, kaida na maadili wanayoshiriki, na sheria na taasisi ambazo hujenga imani na uwiano. Ili kuafikia mabadiliko ya kudumu huhitaji nchi kufuata mwelekeo thabiti na wa usawa wa maendeleo. Hata hivyo, nchi ambazo zimefanikiwa kuwasha ukuaji endelevu katika mapato na maendeleo ya binadamu hazikufuata njia moja rahisi. Zikiwa zimekabiliwa na changamoto tofauti, zilitumia njia mbalimbali kutegemea taratibu za soko, utangazaji wa bidhaanje, maendeleo ya kiviwanda na urekebishaji wa kiteknolojia ili kufaa matumizi fulani na ukuaji. Kipaumbele kinahitaji kuzingatia binadamu, zikijenga nafasi na wakati huo huo zikilinda watu dhidi

KIELELEZO 5


**Kama mgao wa bidhaa za kibiashara ulimwenguni, biashara ya Kusini-Kusini ilipanda kwa zaidi ya mara tatu kati ya 1980-2011, huku biashara ya Kaskazini-Kaskazini ikipungua**




**Kumbuka:** Katika mwaka 1980 Kaskazini inarejelea Australia, Kanada, Japani, Nyuzilandi, Marekani na Ulaya/Uropa Magharibi.
**Chanzo:** Kokotoo za HDRO kutokana na UNSD (2012).

KIELELEZO 6


**Baadhi ya nchi zimefanya vizuri katika vipengele vya HDI visivyo na mapato na viliyo nayo**




**Kumbuka:** Imetokana na kundi lililosawazishwa la nchi 96. Nchi zilizotajwa ni sampuli ya uwakilishaji wa kimaeneo ya watendaji wa maendeleo ya binadamu na zimejadiliwa kwa kina zaidi katika sura yote.
**Chanzo:** kokotoo za HDRO.

KIELELEZO 7


**Thamani ya sasa ya HDI na matumizi ya zamani ya umma vinapatana kwa uhakika....**




**Chanzo:** kokotoo za HDRO na Benki ya Dunia (2012a).

KIELELEZO 8

**. . . kama ilivyo kwa kuendelea kuishi kwa watoto sasa na matumizi ya zamani ya umma kwenye afya**




**Chanzo:** kokotoo za HDRO kulingana na Benki ya Dunia (2012a)

ya hatari za mporomoko wa kiuchumi. Serikali zinaweza kukuza viwanda ambavyo vinginevyo havingeinuka kwa sababu ya upungufu wa masoko. Ingawa hili linaleta hatari za kisiasa za upangishaji na ubarakala, limewezesha nchi kadhaa za Kusini kugeuza viwanda ambavyo mwanzoni vilidhihakiwa kuwa havina ufanisi na kuvifanya kuwa viendesha vilivyofanikisha biasharanje baada ya uchumi wake kuwa wazi zaidi.

Katika jamii kubwa na changamano, matokeo ya sera yoyote ile hutarajiwa yasiwe ya hakika. Mataifa yanayoendelea yanahitaji kuwa ya vitendo, na yajaribu mitazamo mbalimbali. Baadhi ya sifa hujitokeza zaidi: kwa mfano, mataifa yanayoendelea yanayojali watu wake yamepanua huduma za kimsingi za kijamii. Kuwekeza katika uwezo wa watu - kupitia kwa afya, elimu na huduma nyingine za umma – si nyongeza ya mchakato wa ukuaji bali ni sehemu muhimu ya ukuaji (kielelezo 7 na 8). Upanukaji wa kasi wa kazi nzuri ni sifa muhimu ya ukuaji ambao unajenga maendeleo ya binadamu.

## Kiendesha 2: kujinufaisha kutokana na masoko ya dunia

Masoko ya dunia yamekuwa na dhima kubwa ya kuendeleza ukuaji. Nchi zote mpya za kiviwanda zimefuata mbinu ya "kuingiza kutoka nchi za nje kile ambacho ulimwengu unajua na kutoa nje ya nchi kile inachotaka". Lakini kilicho muhimu zaidi ni masharti ya namna ya kufanya kazi na masoko haya. Bila kuwekeza kwa watu, faida kutoka kwa masoko ya dunia haitakuwa kubwa. Kuna uwezekano kuwa mafanikio yatakuwa si matokeo ya kufungua mara moja bali ni matokeo ya utangamano wa taratibu na uchumi wa dunia, kulingana na hali za kitaifa, na ikiandamana na uwekezaji katika watu, taasisi na muundo msingi. Nchi za uchumi mdogo zimesisitiza mazao yanayoleta mafanikio yasiyosahaulika, ambayo huchaguliwa aghalabu baada ya miaka mingi ya usaidizi kutoka kwa serikali yanayojengwa kwenye uwezo uliopo au ukuzaji wa uwezo mpya.

**Kwa nini Mji wa New York ulielekea Kusini kutafuta ushauri wa sera ya kumaliza umaskini**

In New York City, we are working to better the lives of our residents in many ways. We continue to improve the quality of education in our schools. We have improved New Yorkers' health by reducing smoking and obesity. And we have enhanced the city's landscape by adding bike lanes and planting hundreds of thousands of trees.

We have also sought to reduce poverty by finding new and better ways to build self-sufficiency and prepare our young people for bright futures. To lead this effort, we established the Center for Economic Opportunity. Its mission is to identify strategies to help break the cycle of poverty through innovative education, health and employment initiatives.

Over the last six years, the centre has launched more than 50 pilot programmes in partnership with city agencies and hundreds of community-based organizations. It has developed a customized evaluation strategy for each of these pilots, monitoring their performance, comparing outcomes and determining which strategies are most successful at reducing poverty and expanding opportunity. Successful programmes are sustained with new public and private funds. Unsuccessful programmes are discontinued, and resources reinvested in new strategies. The centre's findings are then shared across government agencies, with policymakers, with nonprofit partners and private donors, and with colleagues across the country and around the world who are also seeking new ways to break the cycle of poverty.

New York is fortunate to have some of the world's brightest minds working in our businesses and universities, but we recognize there is much to learn from programmes developed elsewhere. That is why the centre began its work by conducting an international survey of promising antipoverty strategies.

In 2007, the centre launched Opportunity NYC: Family Rewards, the first conditional cash transfer programme in the United States. Based on similar programmes operating in more than 20 other countries, Family Rewards reduces poverty by providing households with incentives for preventive health care, education and job training. In designing Family Rewards, we drew on lessons from Brazil, Mexico and dozens of other countries. By the end of our three-year pilot, we had learned which programme elements worked in New York City and which did not; information that is now helpful to a new generation of programmes worldwide.

Before we launched Opportunity NYC: Family Rewards, I visited Toluca, Mexico, for a firsthand look at Mexico's successful federal conditional cash transfer programme, Oportunidades. We also participated in a North–South learning exchange hosted by the United Nations. We worked with the Rockefeller Foundation, the World Bank, the Organization of American States and other institutions and international policymakers to exchange experiences on conditional cash transfer programmes in Latin America, as well as in Indonesia, South Africa and Turkey.

Our international learning exchanges are not limited to these cash transfer initiatives; they also include innovative approaches to urban transportation, new education initiatives and other programmes.


No one has a monopoly on good ideas, which is why New York will continue to learn from the best practices of other cities and countries. And as we adapt and evaluate new programmes in our own city, we remain committed to returning the favour and making a lasting difference in communities around the world.

## Kiendesha 3: uvumbuzi wa sera ya jamiisocial policy innovation

Nchi chache zimeweza kuendeleza ukuaji wa haraka bila kuwa na viwango vya juu vya uwekezaji wa umma – sio tu katika miundo mbinu, lakini pia katika elimu na afya. Sharti lengo liwe ni kuunda duara za uadilifu na ubora ambamo ukuaji na sera za kijamii zinashajiishana. Mara nyingi ukuaji umekuwa na athari kubwa katika kupunguza umaskini kwenye nchi zenye kutokuwa na usawa katika mapato ya chini kuliko katika nchi zilizo na kutokuwa na usawa katika mapato ya juu. Kujenga usawa, hususan kati ya dini mbalimbali, makabila au vikundi vya kijamii, pia husaidia kupunguza migongano ya kijamii.

Elimu, utoaji wa afya, ulinzi wa kijamii, uwezeshaji wa kisheria na mpangilio wa kijamii, yote huwezesha watu maskini kushiriki katika ukuaji. Usawazishaji wa sekta – hasa kufikiria zaidi juu ya vijiji – na hali na mwendo wa upanuzi wa nafasi za kazi ni muhimu katika kuamua kiasi ambacho ukuaji utasambaza mapato. Lakini hata vifaa hivi vya kimsingi vya sera huenda visiwezeshe makundi yaliyonyimwa haki. Watu maskini walio ukingoni mwa jamii hujitahidi kueleza matatizo yao, na mara nyingi serikali hazifanyi tathmini kuona kama huduma zilizokusudiwa kumfikia kila mtu zimemfikia. Lazima sera ya kijamii iendeleze ujumuishaji – kuhakikisha kuwa hakuna ubaguzi na kuchukulia watu kuwa sawa ni muhimu kwa uthabiti wa kisiasa na kijamii – na itoe huduma za kimsingi za kijamii ambazo zinaweza kuimarisha ukuaji wa muda mrefu wa kiuchumi kwa kuunga mkono mwibuko wa wafanya kazi wenye afya na walioelimika. Si lazima huduma hizi zote zitolewe kwa umma lakini taifa linapaswa kuhakikisha kuwa wananchi wake wote wanaweza kufikia mahitaji ya kimsingi ya maendeleo ya binadamu (angalia kisanduku 3)

FIGURE 9




Kwa mujibu wa maendeleo ya binadamu, gharama ya kutofanya chochote iko juu kwa nchi zenye HDI ambayo ni ya chini kiasi. Kwa mujibu wa hasara ya GDP ya kila mtu, gharama ya kutofanya chochote ina uwiano sawa kwa nchi zote bila kujali kiwango chao cha HDI.

**Chanzo:** kokotoo za HDRO calculations kulingana na Pardee Center for International Futures (2013).

Ajenda ya mabadiliko ya maendeleo inayoendeleza maendeleo ya binadamu huwa na sura nyingi. Inapanua rasilmali ya watu kwa kuwawezesha watu wote kupata huduma za kimsingi. Inaboresha utendakazi wa taifa na taasisi za kijamii ili kuendeleza usawa katika ukuaji ambapo manufaa yamesambaa. Inapunguza urasimu na vikwazo vya kijamii juu ya vitendo vya kiuvhumi na upandaji ngazi kijamii. Pia inawafanya viongozi kuwajibika.

## Kuendeleza msukumo

Nchi nyingi za Kusini zimeonyesha ufanisi mkubwa. Lakini hata katika nchi zenye mafanikio makubwa, ufanisi wa siku za usoni haujahakikishwa. Nchi za Kusini zinawezaje kuendeleza mwendo wake wa ukuaji katika maendeleo ya binadamu, na ni vipi maendeleo hayo yanavyoweza kuenezwa kwenda kwa nchi zingine?Ripoti hii inapendekeza maeneo manne yatakayowezesha hili: kuzidisha usawa, kuwezesha watu kusikika na kuwashirikisha, kukabili shinikizo za kimazingira na kusimamia mabadiliko ya kidemografia. Ripoti hii inabainisha gharama kubwa ya ukimya wa sera na inashawishi kuwepo na utimizaji mkubwa wa sera.

KISANDUKU 4


**Kwa nini matazamio ya idadi ya watu yatatofautiana katika Jamhuri ya Korea na India**

Kiwango cha elimu anachopata mtu kimepanda kwa kasi katika Jamhuri ya Korea. Katika miaka ya 1950, kiasi kikubwa cha watoto wenye umri wa kwenda shuleni hawakupata elimu ya shuleni. Siku hizi, wanawake chipukizi wa Korea ni baadhi ya wanawake wenye elimu bora ulimwenguni: zaidi ya nusu yao wamemaliza masomo ya chuoni.Kwa hiyo, waKorea wazee wa siku zijazo watakuwa na elimu bora kuliko waKorea wazee wa leo (angalia kielelezo). Kwa sababu ya uhusiano dhahiri uliopo baina ya elimu na afya, watakuwa na afya zaidi pia.

Tukichukulia kwamba viwango vya kujiandikisha (ambavyo viko juu) havitabadilika, sehemu ya idadi ya watu walio chini ya umri wa miaka 14 itapungua kutoka 16% katika mwaka 2012 hadi 13% katika mwaka 2050. Pia kutakuwa na badiliko kubwa katika idadi ya watu wenye elimu, ambapo sehemu ya watu yenye elimu ya juu ikikadiriwa kupanda kutoka 26% hadi 47%.

Picha inayojitokeza India ni tofauti kabisa. Kabla ya mwaka 2000, zaidi ya nusu ya watu wazima haikuwa na elimu ya shuleni. Licha ya upanuzi wa hivi majuzi wa masomo ya kimsingi na ukuaji wa kuvutia wa idadi ya Wahindi waliopata elimu bora (bila shaka swala muhimu katika ukuaji wa kiuchumi wa hivi majuzi huko India), sehemu ya watu wazima bila elimu itapungua polepole. Kwa kiasi fulani, kwa sababu ya kiwango hiki cha chini cha elimu, hasa katika wanawake, inakadiriwa kuwa idadi ya watu nchini India itaongezeka kwa kasi, huku India ikiipiku Uchina kama nchi yenye watu wengi zaidi. Hata katika hali ya kutegemea mazuri ya haraka, ambayo inachukulia kuwa kutakuwa na upanuzi wa elimu sawa na ule wa Korea, mgawanyo wa elimu wa India mwaka 2050 utakuwa na kutolingana kwingi, kukiwa na kikundi kikubwa cha watu wazima wasiosoma (hasa wazee). Hata hivyo, upanuzi wa kasi katika masomo ya juu, kwa mujibu wa taswaira hii, utajenga wafanyakazi vijana wenye kisomo kizuri.

Ulinganishaji wa idadi ya watu na mustakabali wa elimu katika Jamhuri ya Korea na India




**Chanzo:** Lutz and KC 2013.

## Kuzidisha usawa

Usawa mkubwa, unaojumuisha kati ya wanaume na wanawake na kati ya makundi, si tu ya thamani kivyake, lakini pia ni muhimu katika kukuza maendeleo ya binadamu. Kifaa kimoja muhimu sana kwa kusudi hili ni elimu, ambayo huongezea watu kujiamini na kuifanya rahisi kwao kupata kazi bora, kushiriki katika mijadala ya umma na kudai kuwa serikali itoe matunzo ya kiafya, ruzuku ya serikali na mambo mengine wanayostahili kupewa.

Elimu pia ina manufaa mengi kwa afya na makadirio ya uhai (kisanduku 2). Utafiti wa Ripoti hii uligundua kwamba elimu ya mama mzazi ni muhimu sana kwa kuendelea kuishi kwa mtoto kuliko mapato ya familia au utajiri ulivyo na kwamba uingiliaji wa sera una athari kubwa pale ambapo mazao ya elimu ni hafifi mwanzoni. Hili lina athari kubwa sana kisera, kwani linabadilisha msisitizo kutoka kwa juhudi za kuongeza mapato ya familia kwenda kwa juhudi za kuboresha elimu ya wasichana.

Ripoti hii inatetea sana utekelezaji wa sera. Taswira ambapo ukuaji unakuwa wa kasi inaonyesha kuwa nchi zenye HDI ya chini zinaweza kusogea kwenda kwa viwango vya maendeleo ya binadamu vilivyofikiwa na nchi zenye HDI ya juu na ya juu zaidi. Kufikia mwaka 2050, HDI inaweza kupanda 52% barani Afrika kusini mwa Sahara (kutoka 0.402 hadi 0.612) na 36% Asia Kusini (kutoka 0.527 hadi 0.714). Uingiliaji kati wa sera katika hali hii utakuwa pia na athari nzuri katika vita dhidi ya umaskini. Kinyume chake ni kwamba gharama ya kutofanya lolote itakuwa ya juu zaidi, hususan katika nchi zenye HDI ya chini, ambazo zitaathirika zaidi. Kwa mfano, kutokutekeleza sera za elimu kwa wote kutaathiri vibaya mihimili mingi muhimu ya maendeleo ya binadamu kwa vizazi vijavyo.

## Kuwezesha watu kusikilizwa na kuwashirikisha

Isipokuwa tu watu washiriki kikamilifu katika matukio na michakato ambayo inaendeleza maisha yao, njia za maendeleo ya binadamu ya kitaifa hazitatamanika wala kuweza kuendelezwa. Sharti watu waweze kushawishi utengenezaji sera na matokeo. Vijana, hasa, wanatakiwa kuweza kutarajia nafasi nzuri na nyingi za kiuchumi na ushirikishwaji wa kisiasa na uwajibikaji.

Kutoridhika kunazidi huko Kaskazini na Kusini huku watu wakitaka kuwepo na nafasi tele za kueleza masikitiko yao na kuathiri sera, hasa kuhusu usalama wa kimsingi wa kijamii. Vijana wapo kati ya walalamikaji ni vijana, kama itikio la ukosefu wa kazi na nafasi chache za ajira kwa vijana waliosoma.Historia imejaa maasi ya umma dhidi ya serikali zisizowajali watu. Hali hii inaweza kuathiri maendeleo ya binadamu kwani vurugu huzuia uwekezaji na ukuaji na serikali za udikteta huelekeza rasilmali upande wa kudumisha sheria na amani.

Ni vigumu kutabiri ni lini jamii zitafika mwisho wa uvumilivu wao. Malalamiko ya umma, hasa ya watu walio na elimu ya shuleni, hulipuka wakati matazamio yanayofifia ya nafasi za kiuchumi yanapunguza gharama ya kujihusisha katika shughuli za kisiasa. Hali hizi za "kushiriki siasa kwa wingi wa juhudi" zinaratibiwa kwa urahisi kupitia njia mpya za vyombo vya habari.

## Kukabiliana na changamoto za kimazingira

Huku tishio la kimazingira kama mabadiliko ya tabianchi, uharibu wa misitu, uchafuzi wa hewa na maji, na maafa ya asilia humwathiri kila mtu, huumiza nchi maskini na jamii maskini zaidi. Tayari mabadiliko ya tabianchi yanazidisha tishio la kimazingira la kudumu, na hasara za mfumo wa ikolojia vinakuwa kikwazo kwa nafasi za kujipatia kipato, hasa kwa watu maskini.

Ingawa nchi zenye HDI ya chini huchangia kwa kiwango kidogo sana mabadiliko ya tabianchi duniani, kuna uwezekano kwamba wao ndio huhisi sana kwa ukosefu wa mvua ya kila mwaka na kuongezeka kwa ubadilikaji wake, hali hii ikiwa na athari mbaya sana kwa kilimo na riziki. Ukubwa wa hasara hii huangazia umuhimu wa kutumia mbinu za kuwezesha watu waongeze uimara wao dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Gharama ya kutofanya chochote itakuwa ya juu sana. Jinsi hatua za kuchukuliwa zitakavyocheleweshwa, ndivyo gharama itakavyokuwa ya juu. Ili kuhakikisha kuna nchi na jamii zenye uchumi endelevu, sera mpya pamoja na mabadiliko ya kimuundo yanahitajika; sera ambayo inafungamanisha maendeleo ya binadamu na malengo ya mabadiliko ya tabianchi katika utoaji mdogo wa hewa chafu, mbinu za kurekebisha tabianchi na utaratibu mbunifu wa umma-watu binafsi kuchangia kifedha.

## Kusimamia mabadiliko ya kidemografia

Kati ya 1970 na 2011 idadi ya watu duniani iliongezeka kutoka bilioni 3.6 hadi bilioni 7. Watu duniani wanapoelimika zaidi, kiwango cha ukuaji wao kitapungua. Matazamio ya maendeleo huathiriwa na muundo wa umri wa idadi ya watu, pamoja na ukubwa wake. Tatizo moja muhimu linaloendelea kuwepo ni uwiano wa utegemezi – yaani, idadi ya vijana na wazee ikigawanywa na idadi ya watu walio katika umri wa kufanya kazi, 15 – 64.

Baadhi ya nchi maskini zitanufaika kutokana na "faida ya demografia" jinsi mgawo wa idadi ya watu wanaofanya kazi utakavyoongezeka, lakini ikiwa tu kuna sera madhubuti ya utendaji. Kwa mfano, masomo ya wasichana nichombo muhimu cha uwezekano wa kuwepo na faida ya demografia. Wanawake walioelimishwa huwa na watoto wachache, wenye afya na walielimishwa vyema. Katika nchi nyingi wanawake walioelimishwa pia hupewa mishahara ya juu kuliko wafanyakazi ambao hawakuelimishwa.

Kinyume chake ni kuwa maeneo ya Kusini yenye utajiri yatakabiliana na tatizo tofauti kabisa. Jinsi watu wao wanavyozeeka, hili linapunguza mgawo wa idadi ya watu wanaofanya kazi. Kiwango cha watu wanaozeeka ni muhimu kwa sababu nchi zinazoendelea zitapambana kuafikia mahitaji ya walw wazee ikiwa bado hao ni maskini. Kwa sasa nchi nyingi zinazoendelea zina nafasi ndogo tu kupata manufaa yote ya faida ya demografia.

Mitindo ya kidemografia si thabiti. Inaweza ikabadilishwa kwa njia isiyo ya moja kwa moja kupitia kwa sera za elimu. Ripoti hii inawasilisha taswira mbili kwa kipindi cha 2010 – 2050: kuna taswira ya kimsingi ambapo wiano wa waliojisajili unabaki ule ule katika kila kiwango cha elimu, na taswira inayoharakisha kufikia lengo ambapo nchi zilizo na viwango vya chini kabisa vya elimu ya msingi vinakumbatia shabaha ya elimu yenye matumaini makuu. Kupungua kwa wiano wa utegemezi kwa nchi zenye HDI ya chini ya taswaira ya kufikia lengo haraka ni zaidi ya mara mbili ile ya taswira ya kimsingi. Sera za elimu zenye matumaini makuu zinaweza kuwezesha nchi za HDI ya wastani na juu kuzuia ongezeko linalotarajiwa katika wiano wake wa utegemezi, ili kufanya mabadiliko yake ya kidemografia kwenda kwa idadi ya watu wazee isiwe ngumu sana.

Kushughulikia changamoto hizi za demografia kutahitaji kuinua viwango vya elimu watakavyofikia huku nafasi za kazi zikiongezwa – kwa kupunguza kutokuwa na kazi, kuendeleza uzalishaji kazi na kuongeza ushirikishwaji wa wafanyakazi, hususan kati ya wanawake na wafanyakazi wazee.

## wala na ushirikiano katika enzi mpya

Mipangilio mipya ambayo inatangazwa na Kusini na wingi unaotokea ni changamoto kwa taasisi zilizopo na michakato katika uwanja wa kitamaduni wa nchi nyingi kushirikiana katika jambo fulani – uchumi, biashara, uwekezaji na afya – wakati mwingine moja kwa moja na wakati mwingine si moja kwa moja kupitia kwa mifumo badalia ya kimaeneo na sehemu za eneo. Utawala wa dunia na maeneo umekuwa ni mchanganyiko wa mipangilio mipya na miundo ya zamani ambayo inahitaji malezi ya namna mbalimbali. Sharti mabadiliko katika taasisi za ulimwengu yakamilishwe na ushirikiano wa nguvu na taasisi za kimaeneo – na wakati mwingine majukumu mapana kwa taasisi za kimaeneo. Lazima uwajibikaji wa mashirika uenezwe kwa kundi kubwa la nchi pamoja na kundi kubwa la washika dau.

Nyingi ya taasisi na kanuni za sasa za utawala wa kimataifa zilikusudiwa ulimwengu ambao hauingiliani na uhalisia wa kisasa. Tatizo moja ni kwamba taasisi hizi haziwakilishi Kusini vilivyo. Ikiwa zitaendelea kuwepo, taasisi hizi za kimataifa zinahitaji kuwa na uwakilishi zaidi, uwazi na zinazowajibika. Kwa kweli, baadhi ya michakato kati ya serikali mbili au sehemu za serikali moja, ingeimarishwa na ushirikishwaji zaidi wa Kusini, ambayo inaweza kuleta rasilmali si haba za kiuchumi, kiteknolojia na kibinadamu.

Katika mambo haya yote, serikali, kama tunavyoelewa, zinahusika na kuhifadhi mamlaka ya kitaifa. Kufuatilia kwa kiasi kikubwa ubora wa mamlaka ya kitaifa kunaweza kutia moyo fikra ya kukosa au kupata. Mbinu nzuri ni mamlaka yenye uwajibikaji ambapo nchi zinashiriki katika ushirikiano wa kimataifa ulio wa haki, unaoongozwa na sheria na wenye uwajibikaji, ambapo watu wanashirikiana katika juhudi za pamoja zinazozidisha neema duniani. Mamlaka ya uwajibikaji pia yanahitaji kwamba mataifa yahakikishie wananchi wake usalama wa haki za binadamu na usalama wa

wananchi. Kwa mujibu wa mtazamo huu, mamlaka huonekana sit u kama haki lakini kama wajibu.

Dunia hii inayobadilika ina maana nzito kwa utoaji wa bidhaa za umma. Maeneo yanayofikiriwa kimataifa kwamba yanahitaji uangalifu wa haraka na ushirikiano ni pamoja na biashara, uhamiaji na mabadiliko ya tabianchi. Katika hali fulani bidhaa za umma zinaweza kupelekwa na taasisi za kimaeneo, ambazo zinaweza kuepuka kutengana ambako kunapunguza kasi ya ukuaji katika mabaraza makubwa ya nchi nyingi zinazofanya kazi pamoja. Hata hivyo, kuongeza ushirikiano wa kimaeneo kunaweza kuwa na ubaya wake – kama kuongeza mambo kwenye hali changamano, yenye safu mbalimbali na taasisi zenye vijisehemu vingi vilivyofumwa pamoja. Kwa hiyo, changamoto ni kuhakikisha kuna "wingi unaoeleweka" – ili taasisi katika viwango vyote zifanye kazi kwa njia ya mpangilio.

Taasisi za kimataifa za kitawala zaweza kuulizwa kuwajibika na mataifa ambayo ni wanachama, ila pia na makundi ya kiraia. Tayari mashirika ya makundi ya kijamii yameshashawishi uwazi duniani na uwekaji wa sheria kwenye misaada, mikopo, haki za binadamu, afya na mabadiliko ya tabianchi. Mifumo ya makundi ya kijamii inaweza sasa kutumia vyombo vya habari vipya na teknolojia mpya za mawasiliano. Hata hivyo, makundi ya kijamii pia yanaulizwa maswali kuhusu uhalali na uwajibikaji wake na yanaweza kuwa na mifumo isiyofaa. Hata hivyo, uhalali wa siku zijazo wa utawala wa kimataifa utategemea uwezo wa taasisi ili kujishughulisha na mifumo ya wananchi na jumuia.

## Hitimisho: washirika katika enzi mpya

Nchi nyingi za Kusini tayari zimedhihirisha kile ambacho kinaweza kufanywa ili kuhakikisha kuwa maendeleo ya binadamu yanafuata njia ambazo ni zalishi na endelevu, lakini zimepiga tu hatua fupi. Katika miaka ijayo, Ripoti inapendekeza hitimisho tano pana:

### Sharti nguvu za uchumi unaoinuka Kusini zipatanshiwe na ahadi kamilifu ya maendeleo ya binadamu

Uwekezaji katika maendeleo ya binadamu yanatetewa si tu katika misingi ya maadili, lakini pia kwa sababu kufanya vizuri katika elimu, afya na ustawi wa jamii ni muhimu ili kupata mafanikio katika uchumi wa dunia ulio na ushindani na nguvu. Hususan, uwekezaji huu unatakiwa kulenga maskini – ukiwaunganisha na masoko na kuongeza nafasi zao za kazi. Ufukara ni udhalimu ambao unaweza na sharti urekebishwe kwa vitendo imara.

Utungaji sera mzuri huhitaji usisitizaji mkubwa katika kuongeza uwezo wa kijamii, sit u uwezo wa watu binafsi. Watu binafsi hufanya kazi ndani ya taasisi za kijamii ambazo zinaweza kutinga au kuongeza uwezo wao wa kukua. Sera ambazo zinabadilisha kaida za kijamii ambazo zinatinga uwezo wa binadamu kama shutuma dhidi ya ndoa za mapema au mahitaji ya mahari, zinaweza kuongeza nafasi za ziada kwa watu binafsi ili kufikia kikomo cha uwezo wao.

### Nchi ambazo hazijaendelea sana zinaweza kujifunza na kufaidika kutokana na mafanikio ya nchi zenye uchumi unaoinuka Kusini

Ulimbikizaji usio na kifani wa akiba za kiuchumi na hazina za utajiri wa kimamlaka kule Kusini pamoja na Kaskazini hutoa nafasi ya kuchapuza ukuaji mpana. Hata kama sehemu ndogo tu ya hazina hii ingetolewa kwa ajili ya maendeleo ya binadamu na umalizaji wa umaskini ingekuwa na athari kubwa. Wakati huo huo biashara ya Kusini-Kusini na mtiririko wa uwekezaji vinaweza kushawishi masoko ya kigeni kwa namna mpya ambazo zitazidisha nafasi za maendeleo, kama kwa kushiriki katika mkufu wa thamani wa kimaeneo na dunia.

Biashara ya Kusini-Kusini inayochipua na hasa uwekezaji ni vitu vinavyoweza kuwa msingi wa kubadili ukubwa wa kutengeneza bidhaa katika viwanda hadi kwa kwa maeneo na nchi

ambazo hazijaendelea. Mipango ya pamoja kati ya Wachina na Wahindi na uwanzishwaji wa uwekezaji katika viwanda Afrika ni kama mwanzo wa nguvu zilizopanuka sana. Mifumo ya uzalishaji ya kimataifa hutoa nafasi kuharakisha mchakato wa maendeleo kwa kuruhusu nchi kuruka hadi kwa vifundo vya uzalishaji ambavyo ni kisasa zaidi.

## Taasisi mpya pamoja na ushirika mpya waweza kusaidia utangamano wa kimaeneo na uhusiano wa Kusini-Kusini

Taasisi mpya pamoja na ushirika vyaweza kusaidia nchi kushiriki maarifa, tajriba na teknolojia. Hivi vinaweza kuambatana na taasisi mpya na zenye nguvu ili kukuza biashara na uwekezaji na kuchapuza kushiriki kwa tajriba Kusini kote. Hatua moja ingekuwa kuanzisha Tume ya Kusini ili kuleta maono ya jinsi uanuwai wa Kusini waweza kuwa nguvu za umoja.

## Uwakilishaji mkubwa wa Kusini na makundi ya kijamii wanaweza kuchapuza maendeleo kuhusu changamoto kubwa za dunia

Kuinuka kwa Kusini kunaongoza kuleta uanuwai mkubwa wa utetezi katika ukumbi wa dunia. Hili linawakilisha nafasi ya kujenga taasisi za utawala ambazo zitawakilisha maeneo bunge yote ambayo yangetumia uanuwai huu kwa njia zalishi katika kutafuta suluhu kwa matatizo ya dunia nzima.

Kanuni mpya ongozi za mashirika ya kimataifa zinahitajika ambazo zitashirikisha tajriba ya Kusini. Kuibuka kwa Kundi la 20 ni hatua muhimu upande huu, lakini nchi za Kusini pia zinahitaji uwakilishaji wa usawa zaidi katika taasisi za Bretton Woods, Umoja wa Mataifa na mashirika mengine ya kimataifa.

Makundi ya kijamii na matapo ya kijamii, yote yakiwa ya kitaifa na kimataifa, yanatumia vyombo vya habari kukuza wito wao kwa utawala wa haki. Kusambaa kwa matapo na kuongezeka kwa majukwaa ya kuzungumzia ujumbe na matakwa kunatoa changamoto kwa taasisi za kiutawala ili kutumia kanuni za kidemokrasia na zinazojumuisha zaidi. Kwa jumla, dunia yenye haki na kutolingana kuchache huhitaji nafasi ya sauti nyingi na mfumo wa hotuba za umma.

## Kuinuka kwa Kusini kunatoa nafasi mpya za kuzalisha ugavi mkubwa wa bidhaa za umma

Ulimwengu endelevu unahitaji ugavi mkubwa wa bidhaa za umma. Maswala ya kidunia yanaongezeka katika idadi na kasi, kutoka kwa kutoa ukali kuhusu mabadiliko ya tabianchi na kutokuwa imara kwa uchumi wa kimataifa hadi vita dhidi ya ugaidi na ueneaji wa nyuklia. Wanahitaji jibu la dunia. Huku katika maeneo mengi ushirikiano wa kimataifa unaendelea kuwa wa polepole – na wakati mwingine ni wa hatari. Kuinuka kwa Kusini kunaleta nafasi mpya za kutoa bidhaa za umma duniani kwa kikamilifu na kwa kufungua maswala mengi ya dunia ya yaliyokwama.

"Mbele ya watu" na "ya binafsi" mara nyingi si sifa za ndani za uzuri wa umma lakini ni mawazo ya kijamii. Kwa hiyo, zinawakilisha uchaguzi wa sera. Serikali za kitaifa zinaweza kuingilia kati wakati kuna ugavi usiotosha katika ngazi ya kitaifa, lakini changamoto za dunia zinapotokea, ushirikiano wa kimataifa unahitajika na unaweza kutokea tu kwa kitendo cha hiari cha serikali nyingi. Kwa kuwa kuna changamoto nyingi, maendeleo katika kuamua kilicho cha umma na kilicho cha watu binafsi yatahitaji uongozi wenye nguvu, uliojitolea kibinafsi na kitaasisi.

*    *    *    *    *

*Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu* 2013 inawasilisha muktadha wa kisasa wa dunia na inatoa mwongozo kwa watunga sera na wananchi ili kupitia mwingiliano unaoongezeka duniani na pia kukabili changamoto zinazozidi duniani. Inaeleza jinsi mamlaka, utetezi na utajiri vinabadilika katika dunia – na inatambua sera mpya na taasisi zinazohitajika kukabili uhalisia wa karne ya 21 na kukuza maendeleo ya binadamu pamoja na usawa mkubwa, uelekevu na utangamano wa kijamii. Kupiga hatua katika maendeleo ya binadamu kunahitaji vitendo na taasisi katika

kiwango cha dunia na kiwango cha kitaifa. Katika kiwango cha dunia, mabadiliko ya taasisi na uvumbuzi huhitajika kulinda na kutoa bidhaa za umma duniani. Katika kiwango cha kitaifa kujitolea kwa ajili ya haki ya kijamii ni muhimu, kama ulivyo uhalisia kwamba sera za teknokrasia ambapo watu wote wanapewa sera zinazofanana, si halisi wala haiwezi kuleta matokeo tukichukulia uanuwai wa miktadha ya kitaifa, tamaduni na hali za taasisi. Hata hivyo, kanuni za juu kama uwiano wa kijamii, ujitoleaji wa taifa upande wa elimu, afya na ulinzi wa kijamii, na uwazi katika utangamano wa biashara huibuka kama namna ya kuongoza chombo kuelekea maendeleo ya binadamu endelevu na yenye usawa.

**Ripoti za Ulimwengu za Maendeleo ya Binadamu:** Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu 2013 ndiyo ya hivi punde katika mfululizo wa Ripoti za Ulimwengu za Maendeleo ya Binadamu zilizochapishwa na UNDP tangu 1990 kama tafiti huru, zenye misingi ya kijarabati kuhusu maswala makuu ya maendeleo, mitindo/mielekeo na sera.
Marejeleo ya ziada yanayohusiana na Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu 2013 yanaweza kupatikana kwenye mtandao katika hdr.undp.org, ikiwa ni pamoja na matoleo makamilifu au muhutasari wa Ripoti hiyo katika lugha zaidi ya 20; mkusanyiko wa Makala za Utafiti wa Maendeleo ya Binadamu zilizoteuliwa kwa ajili ya Ripoti ya 2013; ramani na hifadhidata husishi za viashiria vya maendeleo ya binadamu ya kitaifa; maelezo kamili ya vyanzo na methodolojia zilizotumiwa katika Ripoti za vielezo vya maendeleo ya binadamu; maelezo mafupi kuhusu nchi; na nyenzo nyingine za kimsingi. Ripoti za zamani za Maendeleo ya Binadamu za dunia, kimaeneo na kitaifa zinapatikana pia katika hdr.undp.org.

**Ripoti za Kimaeneo za Maendeleo ya Binadamu:** Kwa zaidi ya miongo miwili iliyopita, Ripoti za Maendeleo ya Binadamu zinazolenga maeneo fulani zimetolewa katika sehemu zote kuu za ulimwengu unaokua kwa msaada kutoka kwenye ofisi za kimaeneo za UNDP. Huku kukiwa na uchanganuzi wa kina na mapendekezo wazi ya sera, hizi Ripoti za Kimaeneo za Maendeleo ya Binadamu zimechunguza maswala nyeti kama uwezeshaji wa kisiasa katika nchi za Kiarabu, upatikanaji wa chakula Afrika, mabadiliko ya tabianchi Asia, utendewaji wa makabila ya walio wachache Uropa ya Kati, na changamoto za kutokuwa sawa na usalama wa wananchi katika Amerika ya Kusini na Carribean.

**Ripoti za Kitaifa za Maendeleo ya Binadamu:** Tangu kutolewa kwa ripoti ya kwanza ya Ripoti za Kitaifa za Maendeleo ya Binadamu, ripoti hizi zimetolewa katika nchi 140 na timu za uhariri za mahali hapo zikiwa zinasaidiwa na UNDP. Ripoti hizi – baadhi yake zikiwa 700 hivi kufikia sasa – huleta mtazamo wa maendeleo ya binadamu katika shughuli za sera ya kitaifa kupitia kwa mashauriano na utafiti. Ripoti za Kitaifa za Maendeleo ya Binadamu zimeshughulikia maswala mengi ya kimsingi ya maendeleo, tangu tabianchi hadi uajiri wa vijana na kutokuwa sawa kunakoongozwa na jinsia na ukabila.

## Ripoti za Maendeleo ya Binadamu 1990–2013

1990 Dhana na Upimaji wa Maendeleo ya Binadamu
1991 Kugharamia Maendeleo ya Binadamu
1992 Mawanda ya Kiulimwengu ya Maendeleo ya Binadamu
1993 Kushiriki kwa Watu
1994 Mawanda Mapya ya Usalama wa Binadamu
1995 Jinsia na Maendeleo ya Binadamu
1996 Ukuaji wa Kiuchumi na Maendeleo ya Binadamu
1997 Maendeleo ya Binadamu Yanayokusudiwa Kumaliza Umaskini
1998 Matumizi Yanayolenga Maendeleo ya Binadamu
1999 Utandawazi Unaozingatia Utu
2000 Haki za Binadamu na Maendeleo ya Binadamu
2001 Kuzifanya Teknolojia Mpya Zifaidi Maendeleo ya Binadamu
2002 Ukitaji wa Demokrasia katika Ulimwengu Uliogawanyika
2003 Malengo ya Kimaendeleo ya Milenia: Ushikamano wa Mataifa Kumaliza Umaskini wa Binadamu
2004 Uhuru wa Kiutamaduni katika Ulimwengu Anuwai wa Sasa
2005 Ushirikiano wa Kimataifa katika Njia Panda: Misaada, Biashara na Usalama katika Ulimwengu Usio na Usawa
2006 Uhaba Uliokithiri: Uwezo, Umaskini na Tatizo Kubwa la Maji Duniani
2008 Kupigana na Mabadiliko ya Tabianchi: Umoja wa Wanadamu katika Ulimwengu Uliogawanyika
2009 Kushinda Vizuizi: Kupanda kwa Binadamu na Maendeleo
2010 Utajiri Halisi wa Mataifa: Njia Zinazoleta Maendeleo ya Binadamu
2011 Uendelezaji na Usawa: Mustakabali Mzuri kwa Wote

United Nations Development Programme
One United Nations Plaza
New York, NY 10017

www.undp.org

Karne ya 21 inashuhudia mabadiliko makubwa katika elimumwendo wa dunia yanayoendeshwa na mataifa mapya yenye uwezo yanayoinukia kwa haraka katika ulimwengu unaoendelea. Nchi ya Uchina imeshaipiku Japani kama nchi ya pili yenye uchumi mkubwa ulimwenguni. Hali hii imewaondoshea mamia ya mamilioni ya watu umaskini. India inapanga upya mustakabali wake ikitumia ubunifu mpya wa kibiashara na uanzishaji wa sera mpya ya kijamii. Brazil inainua viwango vyake vya maisha kwa kupanua uhusiano wa kimataifa na mipango dhidi ya umaskini ambayo inaigwa kote ulimwenguni.

Lakini 'Kuinuka kwa nchi za Kusini' ndilo tukio kubwa zaidi. Uturuki, Meksiko, Tailandi, Afrika Kusini, Indonesia na mataifa mengine yanayoendelea yameanza kuchukua ongozi katika ulingo wa kimataifa. Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya 2013 inatambua zaidi ya nchi 40 katika ulimwengu unaoendelea ambazo zimekuwa na matokea mema kuliko ilivyotarajiwa upande wa maendeleo ya binadamu katika miaka ya hivi karibuni. Maendeleo ya nchi hizi yameshika kasi sana katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.

Kila moja ya nchi hizi ina historia yake ya kipekee na imechagua mkondo tofauti wa maendeleo yake. Hata hivyo, bado nchi hizi zinashiriki sifa muhimu na zinakumbwa na changamoto nyingi zinazofanana. Pia nchi hizi zinafungamana na kutegemeana kwa kiasi kikubwa. Watu walio katika ulimwengu unaoendelea wanazidi kudai kuwa wasikilizwe, wanapopokezana mawazo kupitia kwa njia mpya za mawasilaino na kutaka uwajibikaji mkubwa zaidi kutoka kwa serikali na taasisi za kimataifa.

Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu ya 2013 inachanganua asili na matokeo ya kuendelea *'Kuinuka kwa Nchi za Kusini'*, na inatambua sera zilizokita katika uhalisia huu mpya ambazo zingeweza kusaidia kuleta maendeleo zaidi kote ulimwenguni katika miongo ijayo. Ripoti hii inataka kuwepo na uwakilishaji mzuri wa Nchi za Kusini katika mifumo ya utawala ya kilimwengu na inaonyesha vinavyoweza kuwa vyanzo vipya vya kugharamia bidhaa muhimu za umma katika Nchi za Kusini. Huku ikiwa na utambuzi mpya wa kiuchanganuzi na mapendekezo wazi ya mabadiliko ya sera, Ripoti hii inasaidia kuonyesha mwelekeo kwa watu wa maeneo yote ili wakabili changamoto zinazofanana za maendeleo ya binadamu pamoja kwa namna ya kuridhisha itakayozaa matokeo.

*"Ripoti hii inaleta nguvu mpya katika uelewa wetu wa jinsi hali ya maendeleo ilivyo ulimwenguni, na inadhihirisha kiasi ambacho watu wanaweza kujifunza kutokana na tajriba ya maendeleo ya haraka katika nchi nyingi zilizo Kusini."*

— Msimamizi wa UNDP Helen Clark, kutoka kwa Dibaji

*"Mtazamo wa maendeleo ya binadamu ni hatua kubwa mbele katika zoezi gumu la kuelewa ufanisi na mapungufu ya maisha ya binadamu, na katika kufurahia umuhimu wa fikra na kubadilishana mawazo, na kupitia kwa hayo kuendeleza haki duniani."* — Mshindi wa Tuzo ya Nobel AmartyaSen, kutoka Sura ya Kwanza

*"Hakuna mtu aliye na ukiritimba wa mawazo mazuri. Hii ndiyo sababu New York itaendelea kujifunza kutokana na desturi bora za miji na nchi nyingine."* —Meya wa Mji wa New York Michael Bloomberg, kutoka Sura ya Tatu

*"Mtazamo wa kina wa njia anuwai za kimaendeleo ambazo nchi zinzazoendelea na zenye ufanisi zimefuata hutajirisha menu ya uchaguzi wa sera kwa nchi zote na maeneo."* —mwandishi kiongozi wa Ripoti Khalid Malik, kutoka kwa Utangulizi